**12 Mei 2021** **LSE: PDL**

**Petra Diamonds Limited**

## Matokeo ya uchunguzi wa Kamati Ndogo ya Bodi huru kuhusu ya madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu katika Mgodi wa Almasi wa Williamson nchini Tanzania

### *Taarifa fupi*

Petra Diamonds Limited (“Kikundi”, “PDL”, “Petra” au “kampuni”) leo inatoa matokeo ya uchunguzi wa Kamati Ndogo huru ya Bodi ya wakurugenzi kuhusiana na madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu katika Mgodi wa Almasi wa Williamson ("Mgodi") nchini Tanzania, yaliyoletwa na kampuni ya mawakili ya Uingereza, Leigh Day na Asasi isiyo ya kiserikali RAID. Mgodi huo unaendeshwa na kampuni ya Williamson Diamonds Limited ("WDL"), unaomilikiwa na Serikali ya Tanzania yenye hisa 25% na hisa 75% zinamilikiwa na kampuni ya Petra. Petra aliwekeza hisa WDL mnamo mwaka 2009.

WDL na Petra zimechukulia tuhuma za ukikukwaji wa haki za binadamu uliyotajwa kwa uzito mkubwa. Zimeazimia kufanya uchunguzi ili kupata uelewa kamili wa tuhuma hizo kwa lengo la:

• kuelewa kilichotokea;
• kusaidia upatikanaji wa suluhisho muafaka na la haki, kwa masilahi ya pande zote; na
• kuweka utaratibu wa kutorudiwa maswala yaliyoibuliwa na namna ya kushughulikia.

Taarifa hii inawasilisha matokeo ya uchunguzi wa kamati ndogo huru ya bodi ya wakurugenzi iliyoundwa kuchunguza tuhuma hizo. Pia inatoa maelezo juu ya hatua zilizochukuliwa na WDL na Petra mara tu baada ya kuarifiwa juu ya tuhuma hizo na baada ya uchunguzi

Kulingana na matokeo ya uchunguzi wa kamati huru ndogo ya bodi, kampuni ya Petra inakubali kuwa huko nyuma yalifanyika matukio ambayo kwa bahati mbaya yalisababisha upotevu wa maisha, kuumia na kudhalilishwa wachimbaji haramu, ndani ya eneo la mgodi wa WDL. Matukio hayo yalihusisha kampuni ya Zenith iliyokuwa inatoa huduma za ulinzi hapa WDL, pamoja na Jeshi la Polisi la Tanzania (Tanzania Police Force -"TPF"). Wakati wa uchunguzi, hakuna ushahidi ulioeleza kuwa wafanyakazi wa WDL walihusika moja kwa moja na vitendo hivi.

Kabla ya uchunguzi kukamilika kampuni ilichukua hatua za tahadhari kwa haraka kushughulikia tuhuma zilizoibuliwa, ili kupunguza uwezekan wa matukio mapya. Hatua hizo ni pamoja na:

- Kufungwa kwa kituo cha kushikilia watuhumiwa mgodini
- Uteuzi mpya wa mkandarasi/mtoa huduma wa shughuli za ulinzi.
- Kusimamishwa kazi wafanyakazi waliotuhumiwa
- Kuteua mtaalam na kuandaa mpango kamili wa ushirikishwaji wa wadau na jamii zilizoathiriwa
- Utekelezaji wa taratibu za kushughulikia malalamiko ya jamii kila siku
- kubuni utaratibu wa uchambuzi wa malalamiko unaolenga kushughulikia ukiukwaji wowote wa haki za binadamu katika siku za huko nyuma na zijazo, na kuboresha kituo cha matibabu cha Mwadui

Kama ilivyotangazwa leo, maafikiano yamefikiwa, bila kukubali hatia/lawama, kuhusiana na tuhuma zilizoletwa London ("tuhuma") na kampuni ya mawakili ya Uingereza ya Leigh Day, kwa niaba ya walalamikaji 71 wasiojitambulisha, kuhusiana na tuhuma ya ukiukwaji wa haki za binadamu, yakihusishwa na shughuli za ulinzi katika Mgodi wa Williamson.

Kiwango cha fidia ya usuluhishi kilichokubaliwa ni Paundi za Uingereza milioni 4.3, ambayo itagawanywa na kulipwa kwa walalamikaji kupitia kampuni ya mawakili ya Leigh Day, gharama za wanasheria, na pesa ambazo Petra itawekeza katika programu endelevu kwa muda mrefu ikiwa msaada kwa jamii zinazoishi karibu na Mgodi.

Utaratibu mpya wa kushughulikia malalamiko unafadhiliwa na PDL, na utafanya kazi kuzingatia viwango vya juu kabisa vya kimataifa, kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Umoja wa Mataifa kuhusu ya Biashara na Haki za Binadamu. Utaratibu huo unakusudia kuchambua matukio yote ya ukiukwaji wa haki za binadamu katika mgodi ya siku za nyuma na usoni , na kutoa tozo pale inapobidi.

Kampuni ya PDL itafadhili kampeni ya kupambana na Ukatili wa Kijinsia inayolenga kutoa elimu na taarifa kwa makundi yaliyokabiliwa Zaidi na hatari ya unyanyasaji wa kijinsia. Kampeni hiyo inakusudia kuimarisha uwezo wa serikali, mashirika, na jamii katika kuleta mabadiliko ya kudumu ya utamaduni, uwajibikaji mkubwa na mwamko kwa jamii.

**Peter Hill, Mwenyekiti (asiye Mtendaji) wa Petra Diamonds Limited, alisema:**

*"Kampuni, Bodi na Menejimenti tumehuzunishwa na tuhuma, ambazo zinahusiana na jinsi wachimbaji haramu na wengineo waliopo karibu na eneo la mgodi wa Williamson nchini Tanzania, walivyotendewa, na watoa huduma za ulinzi. Bodi imesikitishwa na upotevu wa maisha, kuumia na kutendewa vitendo vya udhalilishaji ambavyo vimeonekana kuwa vimefanyika karibu na mgodi. Makubaliano yaliyofikiwa na wadai, pamoja na hatua zingine zilizochukuliwa, zinalenga kutoa suluhu na kuzuia uwezekano wa matukio kwa siku zijazo. Hatua hizi ziinaambatana na mtazamo wetu wenye lengo la kutoa suluhisho la haki, kwa maslahi ya pande zote, kwa kuzingatia uelewa kamili wa tuhuma zilizotolewa, wenye usawa na usio na upendeleo wa tuhuma zilizotolewa.*

*Mkurugenzi Mtendaji wa Petra, Richard Duffy, alichukua hatua mara baada ya kufahamishwa juu ya madai hayo mnamo 2020. Bodi ya Petra imeazimia kushughulikia mapungufu yaliyoonekana, na wamechukua hatua za kurekebisha pale inapohitajika ili kupunguza uwezekano wa matukio kama hayo kutokea tena, wakitambua kwamba madini ya kampuni WDL yenye thamani kubwa ni kivutio kwa watu na makundi dhalimu yenye nia ya kujinufaisha kibinafsi "*

***Historia***

Eneo la mgodi wa WDL lina ukubwa wa la 30.6km2 katika mkoa wa Shinyanga, kaskazini magharibi mwa Tanzania, na ni moja ya rasilimali kubwa zaidi ya machimbo ya almasi duniani. Kati ya mwaka 2011 na 2021, shughuli za ulinzi kwenye mgodi zilitolewa na kampuni ya Ulinzi ya Zenith na mnamo 1 Machi 2021 kampuni ya ulinzi ya Zenith ilibadilishwa na huduma hiyo inatolewa na kampuni ya GardaWorld. Katika kipindi chote hicho Jeshi la Polisi la Tanzania pia limekuwa likishiriki kikamilifu katika shughuli za ulinzi na usalama mgodini.

Hata kabla ya Petra kuwekeza hisa zake WDL mnamo 2009, mgodi huo umekuwa ukivamiwa mara kadhaa na wachimbaji haramu. Ingawaje kwa watu wengi, uchimbaji haramu ni njia ya kujiongezea mapato, kuna ushahidi unaoashiria kuwa uvamizi katika mgodi unafadhiliwa na kupangwa na makundi haramu ya biashara ya almasi. Wachimbaji haramu hujiunda kwenye vikundi vidogo, hadi vikundi vikubwa zaidi ya watu 200, na wengine wakiwa na silaha za kombeo, mapanga na marungu. Baadhi ya walinzi wa kampuni ya Zenith walikuwa wakijihami kwa bunduki, na tangu Oktoba 2013 walinzi waliamriwa kutumia risasi za mpira. Jeshi la Polisi la Tanzania lilikuwa na silaha za moto na mabomu ya machozi. Hati ya Makubaliano ilisainiwa kati ya Jeshi la Polisi Tanzania na WDL mnamo Mei 2019, ambapo "Pande zote mbili zilitambua umuhimu wa vitendo vinavyoendana na masharti

ya Kanuni za Hiari za Usalama na Haki za Binadamu, kukuza na kulinda uhuru na haki za msingi za binadamu.” Ijapokuwa wavamizi na wachimbaji haramu walishughulikiwa kwa amani, kumekuwa na matukio kadhaa yanayohusisha vurugu.

### *Tuhuma*

Mnamo mwezi Mei 2020, kampuni ya mawakili ya Leigh Day ilitaarifu Bodi ya Petra na WDL kwamba iliwasilisha maombi ya madai katika Mahakama Kuu ya Uingereza na Wales kwa niaba ya watu 32 wasiotambulishwa kuhusiana na madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu, majeraha na vifo vilivyosababishwa na shughuli za kiulinzi mgodini. Kwa kuongezea, mnamo Novemba 2020 asasi isiyo ya kiserikali ya RAID ilichapisha taarifa inayoelezea madai kama hayo, katika kipindi hicho hicho. Kampuni ya mawakili ya Leigh Day baadaye iliongeza idadi ya wadai ambao hawakutambulishwa hadi kufikia 72 wakati asasi ya RAID ilipanua wigo wa madai yao wenyewe.

Petra iliunda Kamati huru Ndogo ya Bodi inayojumuisha Wakurugenzi Wasio Watendaji wa kampuni kusimamia na kufanya uchunguzi wa madai hayo. Kamati Ndogo ilisaidiana katika uchunguzi wake na mpelelezi mtalaam wa nje (Control Risk) kwa kushirikiana na mawakili Freshfields Bruckhaus Deringer LLP.

Kamati Ndogo imezingatia majumuisho ya mpelelezi wa nje, [**ambaye alifanya]** na ilifanya uchunguzi wa kina, ikiwa ni pamoja na kuwahoji mameneja wa zamani na wa sasa wa WDL na PDL, wajumbe wa Bodi, wafanyakazi wa kampuni ya ulinzi ya Zenith na wawakilishi wa jamii inayozunguka Mwadui. Michakato na shughuli zote mawasiliano ya ndani kati ya WDL na PDL pia zilichunguzwa. **[NB: Uchunguzi huu ulifanywa na mpelelezi mtalaam au Kamati Huru Ndogo??Clarify before printing, it is not very clear in the English text.]**

### *Matokeo ya uchunguzi*

Kamati Ndogo ilipata ushahidi wa matukio mengi ya wachimbaji haramu mgodini, Katika miaka kati ya 2012 na 2020 pekee, kulikuwa na matukio zaidi ya 7,100 mgodini ambayo yalipelekea kukamatwa kwa watu zaidi ya 1,700.

Wakati matukio mengi yalitatuliwa kwa amani, kuna ushahidi kwamba kulikuwa na matukio mengi ya kutumia nguvu kwa pande zote mbili, wachimbaji haramu na walinzi. Matukio haya ya kutumia nguvu wakati mwingine yalisababisha kuumizwa watu pande zote mbili, pamoja na uharibifu wa mali na vifaa, pamoja na magari yanayotumiwa na Jeshi la Polisi la Tanzania pamoja na kampuni ya ulinzi ya Zenith.

Ni vigumu kuelezea kwa usahihi idadi ya matukio, ambayo yalisababisha kupoteza maisha, kuumizwa au kudhalilishwa wachimbaji haramu. Timu ya uchunguzi mara nyingi ilitegemea taarifa chache ambazo wakati mwingine zilipingana. Utofauti huu unaeleweka, ikizingatiwa kuwa ni muda mrefu tangu matukio mengi yalipotokea, pamoja na kwamba matukio mengi yalitokea wakati wa usiku. Changamoto nyingine kwa uchunguzi huo ni kutokuwa na uwezo wa kuthibitisha malalamiko ya wadai kutokana na kutotambulishwa.

Uchunguzi umegundua kuwa katika kipindi hicho kulikuwa na vifo 12 vilivyothibitishwa vya wachimbaji haramu, na kuna uwezekano wa kuwepo wa vifo vya wachimbaji haramu wengine wanne. Ushahidi uliopo ni kwamba kati ya wale 12, wengine waliuawa na walinzi wa kampuni ya Zenith na mmoja aliuawa na Jeshi la Polisi la Tanzania, wakati wa mapigano makali. Katika kisa kimoja, mnamo mwaka 2014 mlinzi wa kampuni ya Zenith alikamatwa baada ya kumpiga risasi mchimbaji haramu na baadaye kufungwa kwa kuua bila kukusudia kufuatia kesi iliyosikilizwa nchini Tanzania. Ukiondoa huyu mtu mmoja aliyetajwa hapo juu, haikuwezekana kubaini ikiwa katika vifo vingine vyovyote walinzi wa kampuni ya Zenith waliwajibika kwa makosa ya jinai. Vifo hivyo viliripotiwa kwa kulitaarifu jeshi la polisi Tanzania, na ikibidi WDL itashirikiana na mamlaka zinazohusika na mashtaka. Uchunguzi pia haukuonesha ushahidi wowote kwamba vifo vilisababishwa na, au wafanyakazi wa WDL walihusika na matumizi ya silaha.

Uchunguzi ulibaini kuwa kampuni ya ulinzi ya Zenith na Jeshi la Polisi la Tanzania pia walisababisha majeraha kadhaa kwa wachimbaji haramu na kwamba walitumia nguvu nyingi kupita kiasi wakati wa mapambano. Rekodi pia zinaonyesha kuwa walinzi wengi wa kampuni ya Zenith na askari polisi pia walijeruhiwa.

Tuhuma zilitolewa kwamba wafanyakazi wa kampuni ya Zenith walibadili silaha zikatumia vipande vya mawe na vipande vya vyuma badala ya risasi za mpira, tuhuma hizi zinahusishwa na tukio moja mnamo mwaka 2016, ambapo mlinzi wa kampuni ya Zenith alifungwa kwa miezi sita, ushahidi unaonyesha kuwa hii inaweza kuwa ilitokea zaidi ya mara moja.

Kabla na wakati wa uchunguzi, tuhuma za unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake eneo la mgodi zilitolewa. Kwa kuzingatia unyeti wa matukio haya waathiriwa wa matukio hayo wanaweza kusita kutoa habari zaidi juu ya tuhuma hizo, kwa hiyo malalamiko haya yatajadiliwa zaidi na wadau wakati wa kuanzishwa kwa utaratibu wa mfumo huru wa kushughulikia malalamiko, sambamba na wakati wa kampeni dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia ambayo itasaidia kulielezea suala hili.

Baadhi ya tuhuma zinahusiana na madai ya kudhalilishwa wachimbaji haramu katika hospitali ya Mwadui inayomilikiwa na kuendeshwa na WDL, ikiwemo kufungwa pingu kwa wagonjwa/watuhumiwa waliopo vitandani. Kwa utaratibu wa kawaida nchini Tanzania maafisa wa polisi wanaruhusiwa kuwalinda watuhumiwa waliokamatwa wakiwa hospitalini na / au kuwafunga wagonjwa pingu ikiwa polisi wataona kuna muhimu wa kufanya hivyo, WDL ilisitisha utaratibu huo katika hospitali ya Mwadui na kutekeleza mabadiliko mengine na maboresho ambayo ni pamoja na watuhumiwa kuwekwa katika wodi binafsi za kuwahifadhi wale walio kizuizini au chini ya ulinzi wa polisi.

Kulikuwa na tuhuma nyingine zinazohusiana na unyanyasaji kwa wachimbaji haramu waliowekwa kizuizini kwenye mahabusu iliyoko mlango mkuu wa kuingia mgodini. Mahabusu hiyo hapo awali ilikuwa ikisimamiwa na kampuni ya Zenith, lakini tangu 2016 imekuwa ikiendeshwa na Jeshi la Polisi Tanzania na sio na WDL kama inavyodaiwa. Uchunguzi umeonesha, kwamba kampuni ya Zenith iliendelea kusimamia mahabusu hata baada ya mwaka 2016. Mahubusu hiyo ilifungwa mnamo 29 Septemba 2020.

Imebainika kuwa uongozi wa WDL ulifahamu hali ilivyokuwa na maelezo ya matukio mengi yaliyohusisha baadhi ya vifo na madai yaliyotolewa mwanzoni mwa miaka ya 2010, yalikuwa yanajulikana kwa uongozi ngazi za juu ndani ya PDL na WDL lakini taarifa hizo hazikuwasilishwa kwenye Bodi ya PDL. Ilifahamika pia kwamba tangu kuundwa kwa Kamati ya Utendaji ya PDL mnamo mwaka 2019, tuhuma na matukio yaliyotokea mwaka 2019 na kupitia Muungano wa Asasi za Kiraia chini ya Mfumo wa Kimberly, hayakuwahi kupelekwa kwenye Bodi. Kamati ya Uchunguzi ilipitia mawasiliano ya mtandaoni ndani ya kampuni, na haikuona taarifa zozote zikipelekwa kwenye Bodi, ikimaanisha kuwa Bodi haikuyajua yaliyotendeka. Kama itakavyodhihirika hapa chini, mifumo wa upashanaji taarifa ndani ya WDL na PDL imebadilishwa, ili kuwezesha utoaji wa taarifa za matukio na uvamizi katika muda sahihi, kupitia mifumo miwili tofauti inayojitegemea, na kwa hivyo kuziwezesha Bodi na ngazi za juu za menejimenti kupata taarifa stahiki.

### *Hatua zilizochukuliwa*

Kampuni ya PDL iliamua kujifunza na kufahamu uhalisia wa matukio ili ichukue hatua stahiki za kutatua matatizo yanayojitokeza. Hatua thabiti zilizochukuliwa na kampuni za WDL na PDL, zikiwemo kuongeza ufanisi wa utekelezai wa taratibu zinazolenga kushughulikia kasoro mbalimbali zilizoainishwa kama ifuatavyo:

*Uongozi na Uwajibikaji*

1. Kutokana na matokeo ya uchunguzi kampuni ilichukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba wahusika wanawajibika. Pamoja na Bodi kujihakikishia kwamba hapakuwa na ushahidi kwamba wafanyakazi wa kampuni ya WDL au PDL walihusika katika matukio hayo,

ni wazi kwamba baadhi ya mameneja hawakutimiza wajibu na majukumu yao, ikiwa ni pamoja na kuzijulisha bodi za wakurugenzi za WDL na PDL. Kwa kuzingatia unyeti wa masuala husika, kutotoa taarifa hizo ni jambo linalosikitisha. Hatua stahiki za nidhamu zimechukuliwa. Aidha, baadhi ya wafanyakazi wa kampuni waliacha kazi na wengine wataondoka pia.

Mfumo wa kupeana taarifa ndani ya kampuni ya WDL na PDL imerekebeshwa ili kuziba mianya na kujenga uwajibikaji, unaowezesha utoaji wa taarifa kuhusu uvamizi na matukio kwa haraka na uwazi zaidi. Marekebesho ya mfumo yanataka taarifa ya tukio lolote ifikishwe kwenye kampuni ya PDL mapema iwezekanavyo, kwa uwazi na kufikishwa kwenye Bodi ya wakurugenzi, na kwenye Kamati za Ukaguzi na Kuhakiki Changamoto, na Kamati ya Jamii, Maadili na Utangamano kupitia mifumo isiyoingiliana.

3. Kampuni ya PDL inatarajia kuteua Mwanasheria Maalumu atakaye simamia masuala ya uongozi, ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kuzingatia sheria na maadili katika biashara, na kutoa miongozo kuhusu shughuli mbalimbali za uendeshaji wa kampuni.

*Kanuni za Hiari katika kutoa Huduma ya Ulinzi na uzinagatiaji wa Haki za Binadamu (Security and Voluntary Principles on Security and Human Rights ("VPSHR"))*

1. Mnamo tarehe 1 March 2021 kampuni iliteua mkandarasi mpya kampuni iitwayo GardaWorld West Security Limited, ambayo ni kampuni tanzu ya kampuni ya Kimataifa ya GardaWorld Group, kutoa huduma ya ulinzi. Mafunzo kuhusu Kanuni za Hiari katika Kuto Huduma ya Ulinzi na uzingatiaji wa Haki za Binadamu (VPSHR) yameandaliwa, na mfumo mpya wa utendaji wa ulinzi, na taratibu mpya za utoaji wa taarifa zimeandaliwa, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa kazi zinavyotekelezwa na mkandarasi pamoja na Jeshi la Polisi ili kuhakikisha kuwa Kanuni za Hiari katika Kutoa huduma ya Ulinzi na uzingatiwaji wa Haki za Binadamu, zinazingatiwa.

2. Kufungwa nyumba iliyotumika kuweka mahabusu mnamo tarehe 29 Septemba 2020.

3. Huduma kwa wagonjwa walioko Hospitali ya Mwadui wanaosubiri kufikishwa mahakamani zimerekebeshwa kufuatia matengenezo ya hospitali baada ya kuongezwa vyumba vya eneo lililotengwa kwa matumizi binafsi. Walinzi na wahudumu wa afya katika kampuni ya WDL wamekumbushwa kuzingatia taratibu zote wanapohudumia wagonjwa walio chini ya ulinzi. Watu wote watakaodai kwamba waliathirika wakati wakiwa kwenye eneo la mgodi na kutibiwa hospitali ya Mwadui wataweza kupata taarifa za matibabu yao.

4. Kutekeleza kampeni ya elimu kuhusu Kanuni za Hiari katika katika kutoa Huduma ya Ulinzi na uzingatiaji wa haki za Binadamu: kampeni hii itawalenga mamenenja na viongozi wa ngazi za juu wa kampuni za Petra and WDL, pamoja na vikundi vyote wa walinzi katika Makao makuu ya Kampuni na migodi iliyoko Tanzania na Afrika Kusini.

5. Kuimarisha Maelezo kuhusu Sera ya Kampuni kuhusu Haki za Binadamu**:** Maelezo ya sera ya Kampuni kuhusu haki za Binadamu yalifanyiwa marekebesho na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 10 Septemba 2020, na ipo kwenye Tovuti ya kampuni https://www.petradiamonds.com/about-us/corporate-governance/business-ethics/. Rejea ya Sera hiyo inaandaliwa upya na Kamati ya SED na itatolewa baadaye mwaka huu, na itahakikisha kwamba taratibu mpya za ufuatiliaji zimeanzishwa na zinazingatia Sera hiyo.

6. Kampuni inatekeleza sera inayolinda watetezi wa haki za Binadamu, ambayo inaweka miongozo inayozuia udhalilishaji, hujuma, ili kujikinda na madhara au uonevu katika siku za usoni.

*Mikutano na Wadau*

1. Kuna umuhimu wa kuajiri Mtaalam atakayekutana mara kwa mara na wadau katika kampuni ya WDL ili kuenga mahusiano bora kati ya kampuni na wadau. Jukumu lake kubwa litakuwa

kuunga mkono jitihada za uongozi wa kampuni kujenga mahusiano bora kati jamii zinazozunguka mgodi na wadau wengineo, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa sahihi na mbinu mpya zitakazo wezesha wadau kukuza mahusiano baina ya pande hizo.

2. Uanzishwaji na utekelezaji wa Mpango Mahususi wa kampuni ya WDL wa kukutana na wadau (Stakeholder Engagement Plan ("SEP")). Mpango mahsusi wa kukutana na wadau utahakikisha kuwa ni wa wazi na unaofikika na jamii inayozunguka mgodi. Mpango huo unawalenga wanajamii, asasi za kiraia, Kamati za Maendeleo, viongozi wa serikali za vijiji/mitaa, Jeshi la Polisi, na viongozi wa kijamii. Mpango Mahsusi umelenga kushughulikia masuala yote muhimu yanayowagusa wadau, ikiwa ni Pamoja na masuala ya ulinzi, haki za binadamu, na maendeleo ya jamii.

3. Kufunguliwa Ofisi Mpya ya Mahusiano na Jamii ndani ya ofisi za Mgodi, itakayohudumia malalamiko, itawezesha wadau kuleta malamiko yao bila kubughudhiwa. Ofisi itasimamiwa na watu wenye mafunzo katika fani ya mahusiano na jamii, na wenye uzoefu wa kufanya kazi na jamii zinazozunguka migodi. Ofisi ikizinduliwa itatoa pia fursa ya kufikiwa kwa kutumia mawasilaiano ya simu, ujumbe wa maandishi na kwa njia za mtandao- Whatsapp.

4. Kuanzishwa kwa Vipindi vipya vya Redio "Kwa Pamoja Tunajali" ("Together we care"): ili kutoa fursa kwa kampuni ya WDL na jamii zinazoizunguka kuwasiliana moja kwa moja na kushughulikia kero zote pamoja, na kupeana taarifa.

*Mfumo wa kupokea Malalamiko (OGM,) na Kuanzishwa Miradi ya Kurejesha Imani na Haki (Restorative projects)*

1. Kufuatia uzinduzi wa mfumo wa kupokea malalamiko toka kwenye jamii, utaratibu huru utaundwa ili kupokea malalamiko hayo katika angazi ya pili (Tier 2). Mfumo huo utachunguza matukio yanayoashiria uvunjifu wa haki za binadamu na kutoa suluhiso pale inapolazimu. Mfumo huo utasimamiwa na jopo la watalaamu huru, litakalo fanya kazi zake kwa kuzingatia misingi ya kimataifa inayotokana na Mwongozo wa Umoja wa Mataifa kuhusu na Biashara na Haki za Binadamu. Madhumuni ya mfumo huo ni kuchunguza na kutoa ufumbuzi wa malalamiko kwa kuzingatia taratibu za kisheria za Tanzania, na ushauri huru wa wanasheria. Kampuni za PDL and WDL zinawahimiza wana jamii wenye malalamiko ya kuvunjiwa haki zao watumie mfumo huo, ambao unatarajiwa kuanza kazi ifikapo mwisho wa mwaka huu. Kampuni hizo zitashirikiana na mamlaka za serikali ya Tanzania katika uchunguzi wowote wa makosa ya jinai, iwapo mtu yeyote atapeleka malalamiko yake kwenye mamlaka husika.

2. Miradi ya kujenga uwezo wa Jamii kiuchumi yenye faida endelevu, itakayotokana na kiasi cha pesa pauni za Kiingereza milioni 1 zitakazotolewa na kampuni ya PDL, itaanzishwa ili kuongeza vipato katika jamii. Miradi hiyo ni Pamoja na:

   a) Upembuzi yakinifu utafanyika kuhusu urasimishaji wa mradi wa wachimbaji wadogowadogo kupitia makinikia yaliyoko Mgodi wa Mwadui (WDM) na mradi wa kilimo cha kibiashara,
   b) Utekelezaji wa miradi hiyo kufuatia upembuzi yakinifu,
   c) Kuanzishwa kwa huduma imara za Afya na Tiba katika jamii,
   d) Kuruhusu wana jamii kuingia katika baadhi ya maeneo ya Mgodi kwa utaratibu maalum kwa madhumuni ya kukusanya kuni au kuchunga mifugo,
   e) Kuanzisha kampeni ya kupinga unyanyasaji wa kijinsia na kutoa msaada wa ushauri nasaha kwa wahanga wa unyanyasaji wa kijinsia.

Kampuni ya Petra italazimika kufanya kazi na jamii Pamoja na watalaam kutoka nje ya kampuni, na asasi ja kijamii katika eneo hili ili kuandaa na kutekeleza miradi yote iliyoainishwa. Taarifa za ziada zitatolewa na kampuni hivi karibuni kupitia tovuti yake.

Wakati wote wa kushughulikia masuala haya lengo limekuwa ni kupata suluhisho la matatizo na kuzuia matukio yasijirudie, tukitaambua kwamba si rahisi kufuta kabisa uvamizi wa mgodi, na kwamba almasi inayochimbwa ni madini yenye umbo dogo, ambayo ni rahisi kutoroshwa na yana

thamani  kubwa ambayo yana uwezo wakubadili hali za Maisha za wana jamii. Bodi ya wakurugenzi ya PDL imedhamiria kuanza miradi iliyoanishwa na itaendelea kufuatilia matokeo ya hatua zote zinatazochukuliwa.

**~ Mwisho ~**

**Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na:**


**Petra Diamonds, London**
Marianna Bowes
Simu: +44 20 7494 8203
investorrelations@petradiamonds.com

**Celicourt (PR Advisor)**
Philip Dennis
Jimmy Lea
Simu: +44 20 8158 5829
Petra@celicourt.uk